

**RISALA YA WANAFUNZI CHUO CHA ARDHI MOROGORO KWA MGENI  
RASMI MAHAFALI YA 41 YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO - TAREHE  
14/04/2023**

**Mhe. Geoffrey Mizengo Pinda (Mbunge), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba  
na Maendeleo ya Makazi;**

Mhe. Fatuma Mwassa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro;

Mhe. Profesa Kihanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Cha Ardhi Morogoro;

Bw. Seushi Mburi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wajumbe wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wakuu na Watendaji wote wa Taasisi na Idara za Serikali mliopo hapa;

Wajumbe wa Menejimenti ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Ndugu Wanahabari kutoka Vyombo Mbalimbali Vya Habari;

Wageni Waalikwa Wote, Mabibi na Mabwana.

**Habari za asubuhi!**

### **Ndugu mgeni rasmi;**

Awali ya yote tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kufika kwako hapa chuoni kwetu CHUO CHA ARDHI MOROGORO, tunatambua kuwa umeacha shughuli zako nyingi za kiofisi na ukakubali kuchukua muda wako kuja kujumuika nasi katika shughuli ya kuwaaga ndugu zetu, kwa pamoja tunasema asante sana na Mwenyezi Mungu akubariki na awe pamoja nawe katika shughuli zako na karibu sana Chuo cha Ardhi Morogoro.

### **Ndugu mgeni rasmi;**

Lengo la risala hili ni kukujulisha kuhusu mfanikio, changamoto, maoni na mapendekezo katika kuboresha hali ya kitaaluma na maisha mengine nje ya taaluma chuoni hapa.

### **Ndugu mgeni rasmi;**

Tunalo tatizo katika chuo chetu la uhaba wa vitendea kazi kwa ajili ya masomo yetu, tunao ukosefu wa maktaba (library) kwa ajiri ya kutunzia vitabu na kujisomea, hali hiyo ya ukosefu wa maktaba imepelekea uongozi [management] wa chuo kubadili chumba kilichokuwa ofisi ndogo kitumike kama maktaba, hivyo basi hali hiyo inatupa wakati mgumu wa kujisomea kwani tunakosa vitabu vya kutosha na nafasi ya kutosha.

Tunao upungufu wa vifaa vya kujifunzia vinanvyorandana na taaluma zetu, kwani vilivyopo ni vichache na kwa taaluma ya mipango miji havipo kabisa. Kwa mfano meza na vifaa vya kuchorea, GNSS Receivers, Total stations, Handheld GPS ili tupate elimu inayoendana na wakati.

Tunao upungufu wa vimbweta vya kujisomea kwenye mazingira ya chuo kwani vilivyopo havitoshi hivyo wanafunzi kufanya majadiliano ya kimasomo (Group Discussion) kwenye mazingira magumu.

Tunayo changamoto ya chumba cha kompyuta (computer lab) kwani chumba kilichopo ni kidogo na chenye kompyuta chache na pia zilizopo zimeharibika na idadi ya wanafunzi imeongezeka ukilinganisha na miaka mingine iliyopita.

Tunayo changamoto ya madarasa, kwani madarasa tuliyonayo ni machache na kupelekea mwingiliano wa vipindi vya masomo na kukosa nafasi ya kusoma vipindi hivyo, kwa sababu ya uchache wa madarasa.

### **Ndugu mgeni rasmi;**

Kwa ujumla, miundombinu ya chuo hiki ni ya zamani pia imechakaa na inapelekea upatikanaji duni wa huduma kama vile maji, mifumo mibovu ya umeme pamoja na ukosefu wa uzio kulizunguka eneo la chuo, Tunaomba kupitia wizara yako kufanya utatuzi juu ya changamoto kama zilivyo elezwa katika risala hii.

### **MAPENDEKEZO:**

**Ndugu mgeni rasmi; Tunayo mapendekezo yafuatayo;**

- Tunaomba kupata jengo la maktaba na kuongezewa vitabu kwa ajili ya kujifunzia.
- Tunaomba kurekebishiwa jengo la kompyuta na kuongezewa idadi ya kompyuta.
- Tunaomba kuongezewa vifaa vya kisasa kama GNSS Receivers, HANDHELD GPS, MEZA ZA KUCHOREA na vifaa vingine vya mipango miji na vijiji ili tupate elimu inayoendana na wakati.
- Tunaomba kuboreshewa na kuongezewa mabweni, madarasa pamoja na darasa maalumu la kuchorea (studio) kwa ajili ya wanafunzi wa kozi ya mipango miji na vijiji.
- Kupitia wizara yako Tunaomba wahitimu wanaomaliza masomo yao kupata ajira ya moja kwa moja kupitia TAMISEMI kama taaluma nyingine mfano Afya na elimu.

**HITIMISHO:**

**Ndugu mgeni rasmi;**

Tunakutakia kila la kheri katika kazi za ujenzi wa taifa na tunaamini matatizo tuliyo wasilisha kwako, katika risala hii yatapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Nasi kwa pamoja tunakushukuru sana kwa kuweza kuonesha moyo wa kujali, upendo na kuweza kufika hapa chuoni kwetu Tunaomba usisite kututembelea mara kwa mara kujua maendeleo ya chuo chetu tukiwa kama sehemu ya familia ya wizara yako pindi unapopata nafasi, Mwenyezi Mungu awe pamoja nawe.

Risala hii imeandaliwa na rais wa Serikali ya wanafunzi [ARISO] Chuo cha Ardhi Morogoro - Ndg. CHACHA SAMWEL MARWA.

.....AHSANTE SANA.....